UNACHOPASWA **KUJUA**

KUHUSU **KIFUA KIKUU**

Kifua Kikuu (TB) ni ugonjwa wa kuambukiza unaosababishwa na bakteria ya Mycobacterium tuberculosis (*M. tuberculosis*). Ni ugonjwa ambao sanasana huathiri mapafu, ingawa unaweza kudhuru sehemu yoyote ya mwili. Unasababishwa na bakteria inayosambaa kupitia hewa wakati mtu mwenye ugonjwa amilifu wa TB anapokohoa, kucheka, kuimba au kupiga chafya. TB ni chanzo kikuu cha magonjwa na vifo katika sehemu nyingi za ulimwengu. Juhudi endelevu za kuangamiza TB katika nchi za ng'ambo na Marekani bado zinahitajika.

Mtu mwenye ugonjwa amilifu wa TB anaweza kuueneza kwa watu walio karibu naye kama vile marafiki, wanafamilia, wafanyakazi wenza, na wanafunzi wenza. Ugonjwa wa TB unaweza kuwa mkali sana na hata kuweza kusababisha kifo. Kwa bahati nzuri, ugonjwa wa TB unaweza kuzuiwa kwa matibabu.

KUHUSU **MAAMBUKIZI YA TB YASIYO NA MADHARA**

Watu walio na maambukizi ya kifua kikuu yasiyo na madhara (LTBI) huwa wameambukizwa bakteria ya *M. tuberculosis*. Baadhi ya watu wenye bakteria ya TB katika miili yao huenda hawatapata ugonjwa amilifu wa TB kamwe. Watu wengine, hasa wale walio na mifumo dhaifu ya kinga na hali zingine zinazowaweka hatarini zaidi, wanaweza kupata ugonjwa amilifu wa TB.

Watu wenye maambukizi ya TB yasiyo na madhara hawajisikii wagonjwa, kwa hivyo mara nyingi hawajui kuwa wana bakteria hiyo katika miili yao. Hawana dalili zozote. Hawawezi kuambukizana. Lakini ikiwa maambukizi yao ya TB yasiyo na madhara yatageuka kuwa ugonjwa amilifu wa TB, bila matibabu, wanaweza kuwa wagonjwa, kueneza TB kwa wengine, na hata kufa.

NYENZO **ZA ZIADA**

Vituo vya Kudhibiti na Kuzuia Magonjwa. (2012). *Kifua Kikuu: Pata Ukweli!* [Brosha]. https://www.cdc.gov/tb/publications/pamphlets/Tuberculosis_Get_the-facts.pdf

Vituo vya Kudhibiti na Kuzuia Magonjwa, Kituo cha Kitaifa cha Kuzuia VVU/UKIMWI, Virusi vya Homa ya Ini, Magonjwa ya Zinaa, na TB. (2014). *Maswali na Majibu Kuhusu Kifua Kikuu [TB]*. https://www.cdc.gov/tb/publications/faqs/pdfs/qa.pdf

Vituo vya Kudhibiti na Kuzuia Magonjwa, Kituo cha Kitaifa cha Kuzuia VVU/UKIMWI, Virusi vya Homa ya Ini, Magonjwa ya Zinaa, na TB. (2014). *TB: Unachohitaji Kujua Kuhusu Maambukizi ya Kifua Kikuu*. https://www.cdc.gov/tb/publications/pamphlets/tb_infection.pdf

Latent TB. Active Concern.
Tuberculosis Program

Idara ya Afya ya Virginia

SIMU: 804-864-7906

FAKSI: 804-371-0248 au 804-416-5178

BARUA PEPE: tuberculosis@vdh.virginia.gov

Tovuti: www.vdh.virginia.gov/tuberculosis/

VDH VIRGINIA DEPARTMENT OF HEALTH

Mpango wa TB wa Idara ya Afya ya Virginia unalenga kuzuia, kutibu, na kuangamiza TB ili kulinda afya na kukuza ustawi wa watu wote katika Virginia.

Kielelezo Kutoka kwa Ofisi ya Mawasiliano ya Picha, Virginia DGS: Kitengo cha Manunuzi na Ugavi

TATHMINI • PIMA • TIBU

MAAMBUKIZI YA TB YASIYO NA MADHARA. HATARI YA UWEZEKANO WA KUSHIKWA NA UGONJWA.

TAARIFA ZA MSINGI KUHUSU MAAMBUKIZI YA TB YASIYO NA MADHARA

Mpango wa Kifua Kikuu
Idara ya Afya ya Virginia

I. TATHMINI

Baini ikiwa unaweza kuwa katika hatari ya maambukizi ya TB yasiyo na madhara

Unaishi au kufanya kazi katika mazingira yenye watu wengi ambapo huenda kuna maambukizi mengi ya ugonjwa amilifu wa TB, kama vile:

- Makazi ya muda mfupi kwa wasio na nyumba
- Taasisi ya marekebisho ya tabia
- Makazi ya kutunzia wakongwe na walemavu

Una mfumo dhaifu wa kinga kwa sababu ya:

- Virusi vya UKIMWI
- Kupandikizwa kiungo cha mwili
- Dawa unazotumia

Umetumia muda na mtu ambaye ana ugonjwa amilifu wa TB

Unatumia dawa za kulevya kwa njia ya sindano

Una dalili za ugonjwa amilifu wa TB, kama vile:

- Kikohozi kinachodumu kwa zaidi ya wiki 3
- Homa
- Maumivu ya kifua
- Kupoteza uzito wa mwili
- Kutokwa na jasho usiku
- Uchovu
- Kupungua kwa hamu ya kula

Ulizaliwa, umekaa kwa zaidi ya mwezi mmoja au kusafiri mara kwa mara katika maeneo ambayo ugonjwa amilifu wa TB hupatikana sanasana, kama vile:

- Afrika
- Asia
- Meksiko
- Amerika ya Kati
- Amerika ya Kusini
- Visiwa vya Karibi
- Ulaya ya Mashariki

Zaidi ya 80% ya wagonjwa wanaougua ugonjwa amilifu wa TB nchini Marekani walikuwa maambukizi ya TB yasiyo na madhara ambayo hayakutibiwa.

II. PIMA

Omba kipimo cha TB

Chaguzi za Vipimo vya TB

Hata kama hujisikii mgonjwa, bado unaweza kuwa na maambukizi ya TB yasiyo na madhara. Ikiwa una hali zozote zilizotajwa hapo awali ambazo zinakuweka katika hatari zaidi, unapaswa kuomba kufanyiwa kipimo cha TB kutoka kwa daktari wako au idara ya afya ya mtaa wako. Unaweza kufanyiwa kipimo cha damu au kipimo cha ngozi; vyote viwili vina maumivu madogo sana. Ikiwa matokeo yako ni chanya, daktari wako ataagiza upigwe picha ya eksirei ya kifua ili kuona ikiwa una ugonjwa amilifu wa TB au maambukizi ya TB yasiyo na madhara. Ikiwa matokeo yako ni hasi na una mfumo dhaifu wa kinga au maambukizi ya hivi karibuni, daktari wako huenda akakuagizia kipimo kingine.

Vipimo vya TB na Chanjo ya BCG

Katika baadhi ya nchi ambapo kuna visa vingi vya ugonjwa amilifu wa TB, chanjo ya kinga inayoitwa bacille Calmette-Guérin (BCG) hutolewa kwa watoto wachanga na watoto wadogo. Hii sio kawaida nchini Marekani, lakini ikiwa ulizaliwa katika nchi nyingine, unaweza kuwa umepokea chanjo ya BCG wakati ulipokuwa mchanga sana. Kama ndivyo, kipimo cha damu cha TB ndicho bora zaidi wakati wa kupima maambukizi ya TB yasiyo na madhara.

Ikiwa umepokea chanjo ya BCG, unapaswa kupimwa kwa kipimo cha damu cha TB. Kipimo cha ngozi kinaweza kutoa matokeo chanya hata kama hujaambukizwa bakteria ya TB.

III. TIBU

Kamilisha Matibabu

Matibabu

Ikiwa kipimo chako cha maambukizi ya TB yasiyo na madhara kina matokeo chanya, kuna chaguzi kadhaa za matibabu zinazopatikana. Daktari wako atapendekeza dawa utakazotumia ili kupunguza hatari yako ya kupata ugonjwa amilifu wa TB. Kumbuka kwamba ugonjwa amilifu wa TB tu ndio unaoambukiza, kwa hivyo hauhatarishi jamaa na marafiki zako ikiwa maambukizi ya TB yasiyo na madhara.

Ni muhimu sana kutibu maambukizi ya TB yasiyo na madhara mara tu unapogunduliwa kuwa nayo. Njia bora zaidi ya kujilinda ni kumaliza dawa zako zote kama ulivyoelekezwa. Njia ya pekee ya kuangamiza bakteria ya TB ni kutumia dawa za TB. Ukiacha kutumia matibabu mapema au kukosa kutumia dawa wakati mwingine, bakteria ya TB inaweza kuzidi nguvu mwili wako.

Baada ya Matibabu

Hata baada ya kukamilisha matibabu, kuna uwezekano kwamba vipimo vyako vya baadaye vitakuwa na matokeo chanya. Unapaswa kuomba daktari wako akupe taarifa ya maandishi inayosema kwamba umekamilisha matibabu yote. Cha kusikitisha ni kuwa, inawezekana kupata TB tena hapo baadaye ikiwa utaambukizwa upya. Dawa utakazotumia zitaangamiza bakteria ya TB katika mwili wako katika wakati huo tu.

Maambukizi ya TB yasiyo na madhara yanaweza kutibiwa haraka. Matibabu yanaweza kuchukua miezi 3-4 tu.

Ikiwa una maswali ya ziada, tafadhali wasiliana na Mpango wa TB wa Idara ya Afya ya Virginia.

804-864-7906